Tofauti na inavyotokea kwa watu mashuhuri wanaokufa na mifupa yao kusalia makaburini, kifo cha Yesu kilikuwa tofauti. Kabla ya kufa alisema kuwa anaweza kuondoa uhai wa mwili wake wa kibinadamu, na kisha kuutwaa tena. Mungu peke yake, ndiye aliye na uwezo wa kufanya tendo kama hili. Kuishi kwake bila kutenda dhambi, miujiza aliyoifanya na kufufuka kwake baada ya mwili wake kukaa kaburini siku tatu, ni uthibitisho tosha kuwa alikuwa ni Mungu katika mwili wa mwanadamu.

Kwa kuwa damu ya Yesu Kristo imeharibu nguvu ya dhambi, mwanadamu akitaka anaweza kushinda dhambi za aina zote. Dhambi hizi ni pamoja na zinaa, uchawi, ushirikina, ufisadi, ugomvi, wivu, hasira, ushoga, ndoa za jinsia moja, ubadilishaji wa jinsia, usagaji, fitina, uzushi, ulevi, ulafi, wizi, madawa ya kulevya, kuangalia picha za ngono, rushwa, punyeto, uongo, kuwasiliana na wafu na kuabudu sanamu (Wagalatia 5:19-21).

Kama vile maambukizi ya virusi vya UKIMWI yanavyoepukika kwa kuziba mianya inayohusika kuvieneza, DAMU ya Yesu iliyomwagika msalabani, ndiyo dawa pekee ya dhambi. "Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12). Damu ya Yesu inashinda dhambi, kwa kumkaribisha Yesu moyoni, kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yako. Anaweza kuingia moyoni mwako, mara tu utakapotubu dhambi zako kwa kumaanisha.

Yesu anao uwezo pia wa kukuweka huru dhidi ya magonjwa, ndoto mbaya na kuteswa na pepo wabaya. Kama unataka kumkaribisha Yesu moyoni mwako, sema na Mungu kwa kutumia maneno yafuatayo. "Mungu Baba, natambua kuwa mimi ni mwenye dhambi na sitaki kuendelea kuishi dhambini. Nisamehe dhambi zangu zote na kunipokea kama mtoto, katika familia yako. Nampokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yangu. Naomba unisaidie kuishi maisha yanayoburudisha moyo wako. Asante kwa kuniokoa na kunipatia uzima wako. Amen."

## WASILIANA NASI

Baada ya kuomba maombi haya, wasiliana nasi ili tufurahi pamoja nawe na kukuelekeza katika kanisa litakalokufundisha jinsi ya kushinda dhambi, magonjwa na kazi zote za Shetani.
Ni mimi **ASKOFU RODRICK MBWAMBO** mwandishi wa kipeperushi hiki.
Utendewe Mema!


## MARANATHA RECONCILIATION CHURCH

**S.L.P 7812 Dar es Salaam, Tanzania**
**SIMU: +255 766 109 285 KWA DAR ES SALAAM.**
**SIMU: +255 689 998 039 KWA DODOMA .**
**Barua pepe: maranathayahwe@gmail.com**


# NI ZAIDI YA VIRUSI



KATIKA huduma yangu ya kulia na wanaolia, nimekutana na vilio vya kutisha vinavyotokana na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Ninapoangalia mateso yanayotokana na virusi hivi, najikuta katika msononeko usio na tiba. Kwa kawaida mateso yanayotokana na virusi hivi, yanaanza kama mwendo wa gari moshi. Ni baada ya kipindi kirefu cha kujiimarisha ndani ya mtu, ndipo virusi hivi vinapomwangusha Mwathirika asiinuke tena! Kama huna uzoefu na mateso yanayotokana na virusi hivi, fuatilia kisa kifuatacho.

Kulingana na maneno ya mashuhuda wa kisa kifuatacho, baba mwenye nyumba ndiye aliyeleta virusi nyumbani. Baada ya miaka kadhaa ya kupambana navyo, vilimnyang'anya uhai wake! Ulipofika wakati wa kushusha mwili wake kaburini, mkewe alizirai kutokana na giza lililokuwa mbele ya maisha yake. Waliokuwa karibu naye walianza kumpepea, ili kupunguza kasi ya mapigo ya moyo wake.

Hali ilipoonekana kutotengemaa, ulipitishwa mchango wa dharura, ili kumwahisha hospitalini. Hata hivyo jinsi mapambazuko yalivyozidi kupokezana na mawio, ndivyo hali yake ilivyozidi kutatizika. Zilipotimia siku za kuanua matanga ya msiba wa mumewe, mjumbe alifika kutoka hospitalini na kusema, "Mgonjwa ametutoka!" Hapo majamvi yakakunjuliwa, kuruhusu awamu nyingine ya maombolezo!

Siku ya mwisho ya matanga ilipofika, ndugu walimvika mtoto mkubwa koti la baba yake na kumwambia; "Wewe sasa ndiwe utakayehusika kulea wadogo zako!" Maneno haya yalifuatiwa na sauti za nyayo za miguu, zilizoashiria kujivua jukumu la kulea mayatima hawa. Baada ya kuondokewa na wazazi wao wawili, nyumba ya mayatima hawa watatu iligeuka kuwa maskani ya vilio, njaa na upweke. Kwa kuwa wote walikuwa ni wanafunzi wa shule ya msingi, walilazimika kufanya vibarua baada ya masomo, ili kujipatia kitu cha kuweka mdomoni. Siku walipokosa kibarua, walijikusanya mbele ya kaburi la mama yao na kusema, "Mama, leo hatuna chakula!"

Kama kope za macho yako hazijazidiwa na machozi, naomba tuangalie kisa kingine, kinachoonesha machungu yanayotokana na virusi vya UKIMWI. Kisa hiki nilikutana nacho mjini Morogoro, baada ya kumaliza mahubiri. Wakati wa nikiagana na watu, macho yangu yalikutana na mwili wa mwanamke uliokuwa juu ya godoro. Mwanamke huyu alikuwa amekonda na kubakia mifupa mitupu. Nilipouliza sababu iliyopelekea kuwa vile, sauti iliyochanganyika na kilio ilinijibu ikisema, "Dada yangu ameathirika!"

Ingawa virusi vya UKIMWI vinaenezwa na watu wa jinsia zote, mwanamke huyu alikuwa anateswa na uzinifu wa mumewe. Wakati mama huyu alipofikia hatua ya kuchungulia kaburi, mume wake alimtelekeza na kumwachia mzigo wa kulea na kulisha watoto sita! Huyu naye baada ya miezi kadhaa ya maumivu na kububujikwa na machozi, ilifika saa ya kutenganishwa na uzao wa tumbo lake. Huku akiangalia giza lililokuwa mbele ya watoto wake, kwikwi zisizokatika zilimkamata na kuchukua uhai wake!

Ingawa virusi vya UKIMWI vinaangamiza maelfu ya watu kila mwaka, viko virusi vibaya zaidi ya hivi. Tofauti na virusi vya UKIMWI ambavyo chimbuko lake lina utata, virusi hivi vya pili ambavyo ndicho chanzo cha matatizo yote yaliyoko duniani ni vya kujitakia. Wakati mateso ya virusi vya UKIMWI yakiishia kaburini, haya ya virusi vya pili vinavyoitwa DHAMBI, yanaendelea hata baada ya kifo! Hivi dhambi ni kitu gani? Kwa maneno rahisi, dhambi ni jambo lo lote mtu analowaza au kulisema au kulitenda, linalopingana na neno la Mungu.

Wakati ulimwengu ukiendelea na jitihada za kutafuta dawa ya UKIMWI, dawa ya DHAMBI ilipatikana karibia miaka 2,000 iliyopita. Mungu ndiye aliyeupatia ulimwengu dawa hii, pale alipomtoa Mwanawe ili awe kafara kwa ajili ya dhambi za wanadamu. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa MWANAWE pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

Mtoto huyu alizaliwa kimiujiza na msichana bikira, aliyepata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Malaika akajibu akamwambia, "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu" (Luka 1:35). Sanjari na kuwa Mwana wa Mungu, Mzao huyu wa bikira alikuwa ni yule mwana-kondoo, aliyeteketezwa madhabahuni badala ya Isaka. "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Yohana 1:29).